**TANZANIA LOCAL GOVERNMENT WORKERS UNION (TALGWU)**

Tarehe 21/12/2021

# TANGAZO LA UUZAJI MAGARI CHAKAVU

Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Tanzania TALGWU kinawatangazia Wanachama wote kuwa kinakaribisha maombi ya ununuzi wa magari chakavu yaliyopo Ofisi za Chama Mikoani. Magari yanayouzwa yanapatikana katika Ofisi za TALGWU Mikoa ya Iringa, Ruvuma, Geita, Simiyu, Mbeya, Singida, Kilimanjaro, Manyara na Njombe

## MAELEKEZO KWA MUOMBAJI

i. Mwanachama yeyote wa TALGWU ana haki ya kuomba kununua magari hayo.

ii. Maombi yote yawasilishwe kwa njia ya barua kwa anuani ifuatayo:-
**KATIBU MKUU TALGWU,**
**S.L.P 16097**
**DAR ES SALAAM.**

iii. Muombaji anapaswa kutembelea na kuona magari hayo kabla ya kuomba kununua.

iv. Muombaji aoneshe bei ambayo yupo tayari kulipia gari kama lilivyo.

v. Kwa muombaji atakayeshinda atatakiwa kulipa kiasi chote alichotaja katika maombi au awamu ya kwanza ya malipo asilimia 70 na baada ya mwezi mmoja atatakiwa kulipa asilimia 30 zilizosalia na kukamilisha uhamishaji wa umiliki ndipo atakabidhiwa gari na kadi.

vi. Kwa magari ya Chama yaliyopo mikoani, kipaumbele ni kwa wanachama kutoka Mkoa husika kwanza kabla wanachama wengine nje ya mkoa.

vii. Muombaji aambatanishe nakala ya hati ya mshahara(salary slip) ya mwezi wa hivi karibuni.

viii. Kwa maombi ambayo yaliwasilishwa kabla ya tangazo hili hayatazingatiwa hivyo basi wanapaswa kuomba tena.

ix. Muombaji ahakikishe kuwa anaweka mawasiliano yake sahihi ambayo ni anuani yake, namba ya simu na Mkoa anakoishi.

x. Kwa maelezo zaidi unaweza kuwasiliana na Ofisi za TALGWU Makao Makuu na Ofisi za TALGWU Mikoa yote iliyotajwa hapo juu ikiwa pamoja na kukagua magari hayo.

xi. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 21 Januari, 2022 saa 9:00 alasiri

**"MSHIKAMANO DAIMA"**

……………………………

***Rashid M. Mtima***

**KATIBU MKUU -TALGWU**